



Cour  
Pénale  
Internationale

International  
Criminal  
Court

ICC-PIDS-FS-02-001/09\_Swa

# Baviktime mbele ya Mahakama



Picha: Ron Haviv/VII

**K**ufwatana na kanuni za Mahakama ya Kimataifa ya Jinai, baviktime (*victimes*) banaweza kutumia Prokire (Procureur) habari kusudi aanze anktete (*enquête*). Kuko tena bitu biwili byenye binaangalia baviktime byenye bilibadilika. Itakuwa turu ya kwanza, mu hadisi ya sheria ya kimataifa yenye kuangaliana na maenfraksyo, baviktime kupatiliwa haki ya kuwa na neno mu masambo na ya kuomba balipiwe. Njo kusema kama tribunale haitabasikiliza tu sawa vile batemwé (*témoins*), lakini tena bataweza kusema mawazo na magumu yabo wakati yoyote ya masambo. Inawezekana bafanye vile kupitia batu benye batabasimamia mbele ya sheria. Na baviktime benye banasikiliziwa na Mahakama sawa vile batemwé (*témoins*) batapata msaada na kuchungiwa.

Kazi ya baviktime mu masambo mbele ya Mahakama ya Kimataifa ya Jinai ni nyongezo ku juhudi na kazi yenye Mahakama iko inafanya kusudi batu benye balifanya maenfraksyo za kabambi (*crimes les plus graves*) zenye kugusa dunia yote baweze kupatiliwa malipizi ya bitendo balifanya. Hii inatokana na kanuni yenye kusema aseme ni saa sauti ya baviktime na mateso yabo inasikiliwa njo sheria kweli inakuwaka imefanyika.

Viktime ni mtu mwenye alipata musiba wala magumu kutokana na kitendo kya enfraksyo kyenye Mahakama inaweza kufuatilia. Bikundi (*organisations*) na taasisi (*institutions*) zenye zinahangaikia maneno ya dini, masomo, usanifu (*art*), sayansi (*sciences*) wala msaada (*charité*), nazo zinaweza kuwa viktime kama bitu byabo bya kazi binabomolewa wala kuharibishiwa. Bajije ba ku Mahakama ya Kimataifa ya Jinai njo batasema ni bitu gani byenye biliharibishiwa wala kubomolewa inafaa kuangalia. Lakini, mu bitu bya kuangalia muko : mateso ya mwili (wala bilonda) na ya akili (wala mawazo) njo kusema saa afia ya akili ya mutu imeharibika kufwatana na byenye aliishi wala byenye aliona, muko tena kupoteza wala kuharibishiwa byashara (*marchandises*) wala bitu.

Kusudi ya kusaidia baviktime, Mahakama iliunda Tawi la ushirikishwaji wa waathiriwa na la malipo (*Section de la participation des victimes et des réparations*), na Kitengo cha msaada kwa waathiriwa na mashahidi (*Unité d'aide aux victimes et aux témoins*); byote biko mu biro ya Grefyé (Ofisi ya Msajili). Ile Tawi la ushirikishwaji wa waathiriwa na la malipo (*Section de la participation des victimes et des réparations*) inasaidia baviktime saa bako banaomba ruhusa ya kuwa na neno mu masambo mbele ya Mahakama wala saa banaomba malipo ya magumu wala musiba balipata, wala mu hizi hali zote mbili. Ile Tawi inasaidia tena baviktime kupata mashauri ya kisheria na kubapangia namuna batakuwa na mutu wa kubasimamia mbele ya sheria. Juu ijuwe na isimulie na kila viktime, ile Tawi ikoinafanya nguvu juu ya kusimulia na kukutanana na bikundi ya baviktime, bikundi yenye haiko ya leta (ONG) na bikundi (*associations*) bingine bya batu bya muinchi wala bya kimataifa byenye habitumikie leta, sana sana mu inchi kwenye Mahakama ikoinafanya kazi zake.

Kitengo cha msaada kwa waathiriwa na mashahidi (*Unité d'aide aux victimes et aux témoins*) inachungaka batemwé (*témoins*), baviktime benye bako banaeleza maneno ku Mahakama na batu bengine benye banaogopa juu balieleza maneno ku Mahakama, tena ile Kitengo inababatiaka msaada juu ya mawazo.

Ile Kitengo inapanaka mashauri, inafundishaka na kupana msaada ku matawi ingine ya Mahakama ku byenye kuangalia namuna gani kuchunga sekirité (*sécurité*) na maisha muzuri ya baviktime na ya batemwé. Ile Kitengo inaangaliaka kwa upekee mahitaji ya batoto, ya bazee, ya bilema na ya benye balifanyiwa bitendo bya busharati ku kinguvu wala benye balitendewa bitendo bya kinguvu juu ni banamuke wala juu ni banaume. Tena ile Kitengo iko na kazi ya kufanya na kutumikisha mipango ya ginsi ya kuchunga batemwé.

## Kuwa na neno

Baviktime banaweza kuwa na neno mu masambo :

- bakitumia Prokirere habari juu ya maenfraksyo za kabambi zenye banasadiki kama zilifanyika;
- bakieleza maneno (kushuhudia) mbele ya Mahakama kama banabaita sawa vile batemwé;
- kwa mafa ya yabo, juu ya kupana mawazo yabo na kusema shida zabo ku Mahakama wakati yoyote ya masambo; ile yote itafanyika mu namuna yenye haiko mubaya ku haki za mwenye kushitakiwa na ku masambo ya haki na ya bila kupendelea. Baviktime banaweza kufanya vile mu bipindi bya kwanza bya masambo (kwa mfano mu ile mkusanyo juu ya kusambisha mwenye Prokirere anaomba ruhusa kwa bajije kusudi aanzishe ankete, wala saa anaomba Mahakama ihakikishe mashtaka yenye banabebesha mwenye kushitakiwa) mu wakati ya kusambisha wala wakati ya apel (appel);
- bakiomba malipo.

Baviktime banaweza kuomba kuwa neno mu kila kipindi ya masambo; inafaa banaandika ile dokima (formulaire) ya kuomba kuitikiwa kuwa na neno. Maombi yote inaangaliwaka na bajije (juges) ba mu chumba (chambre) yenye iko inakata ile maneno. Bale bajije njo banasemaka kama kweli ule mutu alipata shida wala magumu kutokana na kitendo ya enfraksyo ya kabambi (crime) yenye Mahakama inapashwa kufuatilia. Tena bajije batasema ni mu kipindi gani njo baviktime banaweza kusema mawazo na shida zabo na namuna gani.

## Kusimamiwa mbele ya sheria

Baviktime kuwa na neno mu masambo itafanyika mara mingi kupitia mutu mwenye kubasimamia mbele ya sheria. Mara mingi, baviktime habatafanya safari ya kuenda ku makao makuu (siège) ya Mahakama kama habapendi. Benye banabasimamia mbele ya sheria njo batabasemea mawazo na shida zabo ku Mahakama. Baviktime bako na uhuru ya kuchagua mutu mwenye atabasimamia mbele ya sheria. Ule mutu anapashwa kujua sana sheria yenye kuangaliana na maenfraksyo kufuatana na kazi ya avoka, ya jije wala ya prokirere yenye alitumikaka, na kujua muzuri kabisa luga moya mu luga mbili za kazi za Mahakama (Kiingereza ao Kifaransa).

Juu ya kubasaidia kupata mutu wa kubasimamia mbele ya sheria, Mahakama ya Kimataifa ya Jinai itapatia baviktime kartasi kwenye kuko majina za baavoka. Ata kama makuta ya Mahakama juu ya msaada ya kisheria ni za kidogo, Mahakama inaweza kupana msaada fulani ya makuta. Tena, Ofisi ya ushauri wa umma wa waathiriwa (Bureau du conseil public pour les victimes) itakuwa tayari kupatia baviktime msaada ya kisheria bila kulipisha.

Kama baviktime ni bamingi, bajije banaweza kubaomba bachague mutu moya (wala kikundi moya ya batu) mwenye atabasimamia mbele ya sheria, juu masambo ipitike muzuri. Kama baviktime habawezi kujichagulia batu bakubasimia bote pamoya mbele ya sheria, bajije banaweza kuomba grefyé (Greffier) wa Mahakama ya Kimataifa ya Jinai kufanya vile. Kama baviktime habafurahi na batu benye grefyé alichaguwa, banaweza kuomba bajije baangalie ile maneno.

## Kujulishwa

Wakati Chumba ikoinaangalia ombi ya viktime ya kuruhusiwa kuwa na neno na kusema namuna gani ule viktime atakuwa na neno mu masambo ya hali (situation) ao ya afere (affaire) fulani, viktime ataambiliwa maneno yenye imetokea mu kila kipindi ya masambo, ni sawa vile siku za mikusanyo juu ya kusambisha, jijema (décisions) za Mahakama na kila apel (appel).

## Malipo

Baviktime banaweza kuomba malipo ya magumu wala misiba yenye balipata kutokana na bitendo bya enfraksyo za kabambi byenye Mahakama inapashwa kufwatilia. Tena Mahakama ayo peke inaweza kukamata mupango ya kuangalia maneno ya malipo, ata kama baviktime habakufanya ile ombi. Baviktime banaweza kufanya ombi yabo na Mahakama itasema kama maombi yabo itaitikiwa wala apana na itasema ni malipo ya namuna gani. Mahakama inaweza kusema namuna mingi za malipo, sawa vile :

- **fidia (indemnisation)** : mara mingi inakuwaka malipo ya makuta kutokana na magumu wala musiba yenye inagusa akili (mawazo), bitu (wala mali) na mwili. Mule ndani munaweza kuwa malipo kutokana na kuumiziwa ku mwili ao muakili, kupoteza mapato, maumivu fulani, mateso, kuchanganyikiwa akili juu ya mawazo na kupoteza bahati;
- **kurudisha (restitution)** : iko na nia, kama inawezekana, ya kurudisha baviktime mu hali balikuwa ndani mbele ya kupata magumu wala musiba. Inaweza kuwa, kwa mfano, kubarudishia bitu byabo.
- **ukarabati (réhabilitation)** : iko na nia ya kuwezesha baviktime kuendelea kuishi maisha ya kawaida ginsi inawezekana. Ile ukarabati (réhabilitation) inaweza kuwa ndani malipo ya matunzo ya mwili, ya akili (psychologique) wala ya kwa munganga wa bendabazimu, na tena makuta za misaada ku majamaa na misaada ya kisheria, na misaada ingine ya lazima juu ya kurudisha heshima na maisha muzuri ya baviktime.

Mwisho ya masambo, Chumba cha kesi (Chambre de première instance) inaweza kusema aseme mtu mwenye amehukumiwa (kondané) na Mahakama alipe baviktime ba maenfraksyo za kabambi (crimes) zenye zimeonekana kama ni yeye njo alizifanya. Mahakama inaweza kusema mutu alipiwe yeye peke wala kusema malipo ipatiliwe kikundi ya batu, kufwatana na mafa ya baviktime mu hali fulani. Malipo yenye kupewa ku kikundi iko muzuri ju inawezesha kupana msaada ku majamaa wala batu yote pamoya na kupatia tena batu ya zile majamaa namuna ya kuanza tena bupya maisha yabo. Masantre (centres) ao fasi za kupana misaada mbali mbali ku baviktime, kwa mfano, zinaweza kujengewa wala mipango yenye iko na maana ya mfano tu inaweza kukamatiwa. Tena, Nchi zinazounda Mahakama ya Kimataifa ya Jinai (Etats Parties) zilifanyaka Mfuko wala kese ya kusaidia baviktime ba maenfraksyo za kabambi (crimes) zenye Mahakama inapashwa kufwatilia na jamaa zabo, ju ya kubapatia namuna fulani ya malipo ata kama mutu mwenye bamekondané (mwenye alifanya ile makosa) hana mali ya kutosha.